TANGAZO LA SERIKALI NA. 1 LIMETOLEWA TAREHE 4/1/2019

# SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d))*

## AMRI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KAHAMA ("KAHAMA WSSA") (YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama ("Kahama WSSA")(ya Kurekebisha Bei za Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2018.

Tarehe ya kuanza

2. Amri hii itaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Januari 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Kahama WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo-

(a) ifikapo tarehe 30 Aprili 2019 au kabla, Kahama WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) Kahama WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la

Amri hii;

(c) Kahama WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(d) Kahama WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

(e) Kahama WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Kahama WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Kahama WSSA katika siku zijazo.

Kutenguliwa kwa Amri

5. Amri hii inatengua matumizi ya Amri Na. 13-008 ya tarehe 1 Januari 2014 na Amri ya Marekebisho Na. 015-019 ya tarehe 1 Novemba 2015.

## JEDWALI LA KWANZA

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Majumbani | 1,015 | 1,688 | 1,888 | 2,069 |
| Taasisi | 1,235 | 2,060 | 2,320 | 2,540 |
| Biashara | 1,300 | 2,165 | 2,450 | 2,660 |
| Viwanda | 1,400 | 2,327 | 2,601 | 2,850 |
| Magati | 1,235 | 2,000 | 2,000 | 2,000 |
| Migodi | 1,970 | 3,275 | 3,670 | 4,031 |
| Kuosha Magari | 1,880 | 3,125 | 3,493 | 3,800 |

Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 2,500 | Wateja wa Kahama WSSA hawatatozwa tozo ya huduma | | |
| Taasisi | 4,000 | | | |
| Biashara | 4,500 | | | |
| Viwanda | 4,500 | | | |
| Magati | 500 | | | |
| Migodi | 80,000 | | | |
| Kuosha Magari | 4,500 | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Wateja Wapya Wote | Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013 | Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013 | | |

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Institution | 20,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Commercial | 20,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Industrial | 20,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Water Kiosk | 10,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Mining | 200,000 | 200,000 | 200,000 | 200,000 |
| Car Wash | 20,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |

Jedwali Namba 1 (e): Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kumwaga Majitaka katika Mabwawa ya Kahama WSSA (TZS/Ujazo wa Tangi la Gari)

| Ujazo wa Gari | Tozo za Sasa | Tozo Zilidhoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Gari lenye tangi la ujazo wa $10m^3$ | - | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| Gari lenye tangi la ujazo wa $5m^3$ | - | 5,000 | 5,000 | 5,000 |
| Gari lenye tangi la ujazo wa $4m^3$ | - | 5,000 | 5,000 | 5,000 |
| Gari lenye tangi la ujazo wa $3m^3$ | - | 5,000 | 5,000 | 5,000 |

## JEDWALI LA PILI

### MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

| **Kazi Zitakazofanywa** | **Shilingi Milioni** | | | **Mwisho wa Utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | |

*Tangazo La Serikali Na. 1 (linaendelea)*

| **Kazi Zitakazofanywa** | **Shilingi Milioni** | | | **Mwisho wa Utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | |
| **Ukarabati na Mabadilisho** | | | | |
| Kukarabati kilango cha kutekea maji katika bwawa la Nyihogo | 5.00 | 2.00 | 2.00 | 30 Juni 2021 |
| Ukarabati wa visima vifupi | | 20.00 | 20.00 | 30 Juni 2021 |
| Kuondoa matope katika bwawa ila kuongeza ujazo wake | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 30 Juni 2021 |
| Kukarabati mfumo wa kutibu maji | 10.00 | 10.00 | 10.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili tabidimeta (HACH0) na kipimaklorini (HACH) | | 7.50 | | 30 Juni 2020 |
| Kubadili kipimaklorini | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 30 Juni 2021 |
| Kukarabati matangi mawili ya kuhifadhia maji ya bwawa | | 30.00 | | 30 Juni 2019 |
| Kubadili bomba la 4" kwa ajili ya kusafirisha maji ya bwawa | 10.00 | 10.00 | 10.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili pampu za kuongeza nguvu | 110.00 | 60.00 | | 30 Juni 2020 |
| Kubadili ubao wa kutawanya umeme | 1.00 | | | |
| Kubadili mabomba 10 ya chuma | | 10.00 | 10.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili DN 110-250 | 20.00 | 25.00 | 30.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili mabomba ya plastiki Daraja D DN 1"-3" | 20.00 | 10.00 | 7.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga vali kipepeo mpya 6 DN300-750mm | | 45.00 | 45.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga dabo kola 22 za DN 110-250mm PN12.5 | 1.00 | 1.00 | 1.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili dira za malipo ya kabla | 10.00 | 15.00 | 15.00 | 30 Juni 2021 |
| | | | | |
| Kubadili dira mbovu zote kwa kununua dira mpya 250 za 3/4" | | 6.00 | 70.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili dira mbovu zote kwa kununua dira mpya 50 za 1" | 1.00 | 2.00 | 3.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili dira mbovu zote kwa kununua dira mpya 800 za 1/2" | 30.00 | 26.00 | 40.00 | 30 Juni 2021 |

*Tangazo La Serikali Na. 1 (linaendelea)*

| **Kazi Zitakazofanywa** | **Shilingi Milioni** | | | **Mwisho wa Utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | |
| Kubadili ofisi ya ulinzi | | 4.00 | | 30 Juni 2020 |
| Kukarabati jengo la busta, | 1.00 | | | 30 Juni 2019 |
| Kukarabati jengo la pampu | 1.00 | | | 30 Juni 2019 |
| Kukarabati jengo la bwela, | 1.00 | | | 30 Juni 2019 |
| Kukarabati matangi ya kutuamisha maji (Sed Tanks) | 1.00 | | | 30 Juni 2019 |
| Kukarabati jengo la wafanyakazi | | 15.00 | | 30 Juni 2020 |
| Kukarabati jengo la Watumishi | | 15.00 | | 30 Juni 2020 |
| Kubadili meza za ofisis | | | 8.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili vidhibitivolti 8 vyenye uwezo tofauti | | 1.00 | 1.50 | 30 Juni 2021 |
| Kurekebisha mfumo wa kompyuta wa kutolea ankara | | 30.00 | 5.00 | 30 Juni 2021 |
| Jumla ndogo (Ukarabati na Mabadilisho) | 232.00 | 354.50 | 287.50 | |
| Uwekezaji Mpya | | | | |
| Kununua na kufunga sluice gate DN160 20 mpya DN160 | 10.00 | 15.00 | 15.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga sluice gate DN200 20 mpya | 10.00 | 15.00 | 15.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga sluice gate DN250 20 mpya | 10.00 | 15.00 | 15.00 | 30 Juni 2021 |
| Kufunga flap valve 5 | | 1.50 | 1.50 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na Kufunga dira 6 za umeumesumaku kwa ajili ya kupima maji mengi (electromagnetic flow meters) | 72.50 | 81.60 | 78.80 | 30 Juni 2021 |
| Kununua dira za maji 50 mpya za 2" | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua gari mpya moja | | | 90.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua pikipiki mpya 10 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua tarakirishi 8 na tarakirishi mpakato 6 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua mashine mbili za kisasa za kupiga chapa | | 5.00 | 5.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua UPS mpya 5 | | | 2.00 | 30 Juni 2021 |

*Tangazo La Serikali Na. 1 (linaendelea)*

| **Kazi Zitakazofanywa** | **Shilingi Milioni** | | | **Mwisho wa Utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | |
| Kununua pampu mpya ya kutolea maji | | | 3.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua jenereta la akiba kwa ajili ya tangi kuu | | | 50.00 | 30 Juni 2021 |
| Kutanua mtandao wa maji hadi Lugera-Bomage, Mhongolo, Nyashimbi, Mhongolo Magharibi, Mhungula downhill, na Mhungula hill | 280.52 | | | 30 Juni 2019 |
| Kutanua mtandao wa maji hadi Mhungula Mlimani, Mwanva Masaki na Nyakato Mikaratusi | | 231.67 | | 30 Juni 2020 |
| Kutanua mtandao wa maji hadi Kagongwa and Zongomera | | | 293.92 | 30 Juni 2021 |
| **Jumla ndogo (Uwekezaji Mpya)** | **404.02** | **385.17** | **590.22** | |
| **Jumla ya Gharama za Uwekezaji** | **636.02** | **739.67** | **877.72** | |

**JEDWALI LA TATU**

**VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)**

| **Maelezo** | **Uniti** | **Lengo la Utendaji** | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** |
| Idadi ya wateja wapya wa maji safi | Na | 1,786 | 1,986 | 1,757 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | **%** | 14 | 14 | 14 |
| Wateja wenye Dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 90 | 90 | 90 |

Dodoma,
......................, 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*